# Dhima ya Tafsiri katika Kuleta Umoja, Uwiano, Amani na Maendeleo nchini Kenya

*Sheila Ryanga* na *Nancy J. Ngowa*

**Ikisiri**

Fujo, vita na uhasama uliibuka nchini Kenya baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2007. Huenda kuna sababu nyingi zilizochangia vurugu hizi, lakini inaaminika kwamba, mojawapo ya sababu hizi ni ukabila. Jambo moja linalodhihirisha makabila ni lugha. Makabila tofauti huongea lugha tofauti. Hata hivyo, tofauti za kikabila zinaweza kukabiliwa iwapo kutakuwa na lugha inayoeleweka kwa kila mtu. Lugha hii pia inafaa iwe ya kienyeji ndiyo watu waweze kujinasibisha nayo na kuielewa vyema (Thiong'o, 1992). Suluhu ni lugha ya Kiswahili. Lugha hii inaweza kuendeleza mbele nchi hasa katika kuleta umoja, uwiano na maendeleo. Makala haya yananuia kutambua jinsi tafsiri za Kiswahili za kazi mbalimbali zinavyoweza kuchangia katika maendeleo ya sekta mbalimbali na kuleta uhusiano mwema nchini Kenya. Pia, yatatoa mwangaza kwa serikali ya Kenya kuhusu mbinu mojawapo ya kuleta umoja, uwiano, amani na maendeleo kwa kuhusisha tafsiri za Kiswahili.

## 1.0 Utangulizi

Lugha ya Kiswahili ilipewa hadhi kubwa mnamo mwaka 2010 kwa kuingizwa kwenye katiba mpya nchini Kenya kama lugha rasmi. Hii inamaanisha kwamba, lugha hii sasa inaweza kutumika katika shughuli zozote rasmi. Hali hii imeongeza umaarufu wa lugha hii. Kutokana na hadhi na umaarufu huu wa lugha ya Kiswahili, ni dhahiri kwamba inaweza kutumika kwa mapana kama chombo cha maendeleo na uhusiano mwema wa watu nchini Kenya.

Baada ya uchaguzi mkuu nchini Kenya mnamo mwaka 2007, kulizuka mapigano baina ya makabila. Watu wengi waliuawa na wengine kufukuzwa kwenye makazi yao na walitakiwa warudi walikotoka (kwenye makazi ya asili); kwamba walikoishi hakukuwa kwao. Ni bayana kwamba vurugu hii ilichangiwa na kutokuwapo kwa upendo na umoja baina ya makabila. Haya yote yalichagizwa na kutokukubaliana na matokeo ya uchaguzi. Inaaminika kwamba, hakukuwa na uwazi katika uchaguzi huo. Hali hii ilizusha uhasama wa hali ya juu. Hata hivyo, inaaminka kwamba, uhasama huu ulikuwa umejificha tangu zamani na ulikuwa ukingojea tu mlipuaji.

Ilibidi kuwe na suluhisho. Kiongozi wa Umoja wa Mataifa; Koffi Annan alikwenda Kenya ili kuingilia kati na kutafuta suluhisho. Hatua muhimu zaidi katika shughuli hii ilikuwa kupanga mikakati ya makubaliano au ajenda za kuzingatiwa ili mapigano na fujo kama hii isirudiwe tena. Mojawapo ya ajenda hizi ni kuhakikisha kunakuwa na umoja, uwiano na uhusiano mwema baina ya watu wa Kenya.

Makala haya yanaangazia mbinu za kuleta umoja, uwiano, amani na uhusiano mwema katika nchi ya Kenya kwa kujaribu kuondoa uhasama baina ya makabila na kuweka mikakati ya kuunganisha makabila kwa kuzingatia mbinu ya tafsiri katika lugha ya Kiswahili. Makala yananuia kuangazia dhima ya tafsiri nchini Kenya katika harakati za kuvunja pingu za ukabila zilizosheheni.

## 2.0 Dhana ya Tafsiri

Tafsiri ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine (Mwansoko na wengine, 2003). Tafsiri huwa na lengo la kupitisha ujumbe kikamilifu. Mpokezi wa ujumbe sharti aelewe kinachozungumzwa ndiyo kuwe na ufanisi wa tafsiri hiyo. Tafsiri ambayo inatilia maanani ujumbe sharti izingatie vigezo vya mawasiliano. Vigezo vya mawasiliano huhitaji uwakilishi, upokezi, uthamini na ukubalifu wa ujumbe katika jamii pokezi. Jambo jingine la kutiliwa maanani kabla ya kutafsiri kazi mbalimbali ni kuzingatia tajriba za kijamii na kitamaduni za lugha pokezi. Haya yote yanapoangaziwa kunakuwa na ufanisi katika tafsiri na ujumbe unaweza kueleweka vilivyo.

## 3.0 Dhana ya Umoja na Uhusiano Mwema katika Jamii: Mtazamo wa 'Ubuntu'

'Ubuntu' ni istilahi inayotokana na lugha za Kibantu za Afrika Mashariki inayorejelea hali ya watu wanaohusiana kuwa na wajibu wa kuheshimu wengine na kuwa na uhusiano mwema (Dion, 2006). Naye Tutu (1999) anaeleza kwamba mtu mwenye 'ubuntu' ana uwazi na kila wakati anasaidia wenzake na kuwapa moyo. Mtu kama huyu hatishwi na ufanisi wa wengine, bali anajiamini na kuona fahari kwamba, yeye ni mtu wa jamii yake nzima. Mtu mwenye 'ubuntu' hafurahii kuona binadamu wenzake wanateseka. Zaidi ya hayo, Tutu anasisitiza kuwa mwanadamu hawezi kuishi peke yake. Mtu anasemekana ana utu iwapo anashirikiana na watu wengine na ushirikiano huu utadhihirishwa na ukarimu wake.

Nelson Mandela katika maelezo yake ya 'ubuntu' kama alivyonukuliwa na Tutu (1999) anasema kwamba iwapo mtu angekuwa anasafiri vijijini, hangehitaji kuomba chakula, bali watu wangempatia chakula na kuhakikisha kuwa anastarehe. Anaendelea kusema kuwa, 'ubuntu' haumaanishi kwamba watu wasijithamini na kujiendeleza, bali wanapofanya hivyo wahakikishe kwamba jamii nzima imefaidika. Ni dhahiri kwamba, 'ubuntu' unasisitiza umoja katika jamii na ile hali ya kujali maslahi ya wengine. Watu wanatakiwa wawe wanajali wenzao katika jamii na waendelezane. Ili mtu katika jamii aweze kumwendeleza mwingine ni sharti awe anampenda na kumthamini.

Kwa upande mwingine, inaonekana bayana katika wimbo wa taifa wa Rwanda na Burundi kwamba 'ubuntu' ni kule kuwa na utu na ukarimu kwa watu wote. Wanaposema *'gira ubuntu'* wanamaanisha kule kufikiria wengine, kuwaonea huruma na kuwa na ukarimu na utu. Wanaposema *'igikoko inyamaswa'* wanamaanisha kwamba, mtu asiye na huruma ni mnyama. Nchi hizi mbili zinaonesha kwamba, zinathamini utu wa wanadamu na kuhakikisha kwamba, kila mara mtu anapoimba wimbo wa taifa aweze kukumbuka mambo haya muhimu. Hata hivyo, hali hii ilikiukwa mnamo mwaka 1994 ambapo kulikuwa na mauaji ya kikabila na kinyama nchini Rwanda. Mauaji haya yalikuwa kinyume na maelezo ya wimbo wa taifa wa nchi hiyo na kinyume cha ubuntu.

Katika nchi ya Uganda, makabila ya Nyankore, Nyoro, Toro na hata Luganda, 'obuntu' inamaanisha kuwa na ukarimu na wema. Nako nchini Tanzania, makabila ya Haya, Nyambo na mengine, neno 'obuntu' lina maana moja na yale makabila ya Uganda. Kwa upande mwingine, mataifa ya magharibi pia yamesisitiza sana umuhimu wa 'ubuntu' katika jamii. Katika mwaka 2009, wakati wa kuapishwa, Elizabeth Frawley Barley, mwakilishi wa *Global Partnership Initiative (Office of the Secretary of State*) nchini Marekani alisema kwamba, katika idara yake angeleta watu kutoka maeneo tofauti na sekta mbalimbali ili kufanya kazi pamoja na waweze kufanikiwa pamoja. Aliita hali hii '*Diplomasia ya ubuntu.*' Naye Bi. Hillary Clinton, Katibu wa nchi, Marekani aliongezea dhana hii ya ubuntu katika usemi wake mashuhuri katika ukumbi huo huo kwamba 'inahitaji kijiji kizima ili kumlea mtoto.'

Zaidi ya hayo inabainika kwamba, maudhui makuu katika filamu ya John Boorman ya mwaka 2004 inayoitwa '*In My Country*' ('Katika Nchi Yangu') ni 'ubuntu.' Filamu hii inasisitiza umuhimu wa utu katika jamii. Katika mkutano wa *'UN World Summit on Sustainable Development'* uliofanyika mwaka 2002 mjini Johannesburg, Afrika Kusini, maudhui makuu pia yalikuwa ni 'ubuntu'. Hivi karibuni kabisa kumefunguliwa tovuti ya Afrika Kusini inayotumia jina 'ubuntu' ili kueleza jinsi watu wanavyoweza kuungana ili kununua bidhaa pamoja na kwa bei nafuu. Kutokana na dhana ya umoja kwa kurejelea 'ubuntu' imedhihirika kwamba, kule kujali masilahi ya wengine ni muhimu sana maishani na watu wanahimizwa kuwa na umoja wa hali ya juu. Jambo hili la 'ubuntu' linasisitizwa kote ulimwenguni kama inavyobainika. Hili ndilo ambalo tunalisisitiza katika makala haya.

## 4.0 Nguvu Zinazoletwa kwa kuwa na Umoja; mfano wa Mnara wa Babeli

Nguvu za nchi na maendeleo huletwa na umoja wa watu na uhusiano mwema. Umoja wa wananchi unaletwa na kuzungumza lugha moja. Kuzungumza lugha

moja huleta nguvu za kipekee kama inavyodhihirishwa katika Biblia, sehemu inayoelezea ‘Mnara wa Babeli’: **(**Mwanzo, 11:1-9):

> Nchi yote ilikuwa na lugha moja na usemi mmoja. Ikawa watu waliosafiri pande zote za mashariki waliona nchi tambarare katika nchi ya shinari; wakakaa huko. Wakaambiana, haya na tufanye matofali tukayachome moto. Walikuwa na matofali badala ya mawe na lami badala ya chokaa. Wakasema, haya na tujijengee mji na mnara na kilele chake kifike mbinguni tujifanyie jina ili tusipate kutawanyika usoni pa nchi yote. Bwana akashuka ili aone mji na mnara waliokuwa wakiujenga wanadamu. Bwana akasema, tazama watu hawa ni taifa moja na lugha yao ni moja na haya ndiyo wanayoanza kuyafanya, wala sasa hawatazuiliwa neno watakalokusudia kulifanya. Haya na tushuke huko tuwachafulie usemi wao ili wasisikilizane maneno wao kwa wao.

Kutokana na nukuu hii inadhihirika kwamba, watu hawa waliokuwa wanazungumza lugha moja na kuamua kujenga mnara kwa pamoja wangekuwa na ufanisi mkubwa. Ule umoja wao hasa katika usemi na matendo ungeleta ufanisi wa kipekee. Ufanisi huu hauna kikomo kama inavyodhihirika pale ambapo mnara huo ungefika mbinguni (usingekuwa na kikomo). Umoja na matendo ya watu hawa unamstaajabisha Mungu, ambaye anashuka kwa madhumuni ya kuja kuona mnara huo ambao walikuwa wakiujenga. Mungu anatambua kwamba, watu hawa wanazungumza lugha moja. Kwa hivyo, kwao hakuna lisilowezekana; wanaweza kufanya chochote wanachotaka. Wakati huo ndipo Mungu anaamua kuwatawanya kwani anatambua kuwa wanachodhamiria kufanya kinawezekana kwa sababu ya umoja na nguvu zinazoletwa na kuzungumza lugha moja.

Kutokana na dondoo hili la Biblia ni bayana kuwa nguvu ziletwazo na kuzungumza lugha moja ni za kiwango cha juu; cha kuweza kumfikia Mungu. Nguvu hizi ndizo zinazoweza kuleta ufanisi katika sekta mbalimbali za nchi iwapo wananchi watazungumza lugha moja na wanafanya mambo kwa pamoja. Katika muktadha wa nchi ya Kenya, ni bayana kwamba lugha ya Kiswahili ndiyo mwafaka zaidi katika kuleta umoja huu (Chimerah, 1998). Kiswahili ni lugha yenye wazungumzaji na wafuasi wengi hasa katika serikali na uwanja wa kiakademia.

### 4.1 Kwa nini Lugha iwe Kiswahili?

Matamanio ya Waafrika yafaa yaelezwe kwa kutumia lugha za Kiafrika (Roscoe, 1977). Lugha ya Kiswahili ni mwafaka kutumiwa nchini Kenya kama lugha ya kuleta umoja, uhusiano mwema na maendeleo. Hii ni kwa sababu ni lugha ambayo inazungumzwa na watu wengi; kwani hufundishwa katika shule za msingi, sekondari na vyuoni. Zaidi ya hayo, Kiswahili hufundishwa kama somo la lazima nchini Kenya. Hivyo, wananchi wote wanaosoma nchini Kenya hivi sasa huweza kuzungumza Kiswahili vizuri. Kiswahili kinazungumzwa na watu takriban milioni mia moja katika Afrika Mashariki na Kati; kwa hivyo ni lugha ambayo ni maarufu nchini Kenya na nchi jirani. Mwandishi mashuhuri Wole Soyinka anasema

kwamba, Kiswahili kinafaa kupewa hadhi zaidi ya ile ya *lingua franca* (Chimerah, 1998). Wole Soyinka anaendelea kusema kwamba, lugha ya Kiswahili imefuzu kuwa lugha ya bara la Afrika. Kama lugha ya Kiswahili inaweza kupendekezwa kama lugha ya bara la Afrika, kwa nini isiwe mwafaka katika nchi ya Kenya? Isitoshe umaarufu wa lugha ya Kiswahili umeendelea hadi ughaibuni. Kiswahili kinafundishwa kama lugha ya kigeni katika nchi nyingi ulimwenguni (Bamgbose, 1991).

Zaidi ya hayo, Kiswahili ni lugha ya Kibantu (Mbotela, 1999). Inabainika kwamba nchi ya Kenya imesheheni Wabantu. Ni bayana kwamba, wananchi wa Kenya wanapozungumza lugha ya Kiswahili ni kama wanazungumza lugha yao ya asili. Ni lugha wanayoweza kujitambulisha nayo. Lugha ya Kiswahili imeelezwa kama lugha ya wenyeji wa Afrika Mashariki (Topan, 2008). Ni muhimu kutambua kwamba, Kenya ni nchi yenye makabila mengi. Githiora (2008) anasema kwamba, Kenya ni nchi yenye idadi kubwa ya watu ambao wametoka makabila mbalimbali. Hata hivyo, lugha ya Kiswahili haizingatii na wala hainasibishwi na ukabila (Were, 2002). Ni rahisi kutumiwa na huwa ina uwezo wa kukopa maneno kutoka lugha nyingine na kuyaswahilisha na kutumika vilivyo.

Ni muhimu kutambua kwamba viongozi mashuhuri wa Afrika, kama vile Nyerere, Kaunda, Nkrumah, Kenyatta, Lumumba, Mandela na wengineo wametambulishwa na lugha ya Kiswahili. Nao Umoja wa Mataifa ya Afrika (AU) ulitambua Kiswahili kama lugha rasmi ya biashara. Katika eneo la Afrika Mashariki, kufufuka kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi za Maziwa Makuu kunategemea Kiswahili, hasa katika uwanja wa biashara, elimu na mawasiliano (Mukasa, 1998). Nchi ya Kenya iko katika harakati za kujitafutia utambulisho wa pamoja kama serikali ya kisasa (Githiora, 2006). Lugha inayoweza kuleta ufanisi huu ni Kiswahili.

## 5.0 Utekelezaji wa Nguvu za Umoja nchini Kenya

Nguvu zinazoletwa na usemi mmoja zinaweza kutekelezwa kwa njia mbalimbali nchini Kenya. Makala haya yananuia kulenga uwanja wa tafsiri za kazi mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili kama njia ya kuleta umoja, uhusiano mwema na maendeleo nchini Kenya. Ni dhahiri kwamba, kazi nyingi za asasi, mashirika, makampuni na sekta mbalimbali za serikali zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Baadhi yake ni vyombo vya habari, bunge, asasi za tiba, sheria, mahakama, elimu, kilimo, uchumi na shughuli za serikali. Sababu kuu ya kuandikwa kwa kazi za asasi hizi kwa lugha ya Kiingereza ni kwamba, Kenya ilitawaliwa na Mwingereza kwa hivyo ikawa inarithi ule uzungu katika kila sekta ya nchi.

Hata hivyo, ni bayana kuwa kazi hizi mbalimbali zitaeleweka vyema iwapo zitatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha ya wenyeji. Ngugi (1993)

anasisitiza kwamba, mambo yanapoandikwa katika lugha ya wenyeji hueleweka zaidi. Kazi za mashirika mbalimbali zinapotafsiriwa zitaweza kueleweka waziwazi kwa wenyeji na jambo hili litashirikisha kila mmoja.

Katika nchi ya Kenya kuna makabila mengi. Wengi wa watu hawa huwa wanaelewa lugha ya Kiswahili kwa sababu,hujifunza lugha hii shuleni na wengine kutoka kwa wenzao. Lugha ya Kiswahili imekuwa ya kila mmoja nchini Kenya. Katika nchi ya Tanzania, Rais Nyerere alitumia lugha ya Kiswahili ili kuondoa dhana ya ukabila na kuleta umoja kati ya wananchi (Topan, 2008). Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili inaweza kuleta umoja wa hali ya juu na uhusiano mwema pamoja na maendeleo nchini Kenya iwapo kazi zote zitatafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili.

Baadhi ya maeneo ya kutafsiriwa yaliyojadiliwa katika makala haya ni pamoja na elimu, masuala ya tiba, vyombo vya habari, sheria, teknolojia na dini. Katika upande wa elimu, inapendekezwa pia kwamba nyanja zote za elimu zifundishwe kwa lugha ya Kiswahili. Hali hii itahitaji kufanyika kwa tafsiri ya istilahi za masomo haya yote kwa lugha ya Kiswahili. Kiswahili kiwe somo la lazima katika hatua zote za elimu hadi vyuo vikuu. Walimu na wahadhiri waweze kufundishwa lugha ya Kiswahili ili waimudu na waendeshe shughuli zote za vyuo kwa lugha ya Kiswahili. Zaidi ya hayo, utafiti uwe mstari wa mbele, hasa vyuoni kuhusu istilahi mbalimbali zitakazoshughulikia nyanja mbalimbali za masomo. Kamusi za tafsiri na istilahi za Kiingereza kwa lugha ya Kiswahili zinazoshughulikia masomo mbalimbali ziandikwe ili zirahisishe kazi hii na masomo yatakayofundishwa.

Kwa upande mwingine, mitambo ya teknolojia kama tarakilishi zitumie lugha ya Kiswahili ili kila mtu aweze kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi, kielimu na kiutamaduni. Hali hii inazuia kuwako kwa wivu kati ya wanaofaidika na lugha hiyo na wale wasiofaidika. Kuwapo kwa programu za kutafsiri katika mtandao huwezesha masuala mbalimbali katika mtandao kutafsiriwa ili watumiaji waweze kuyapata katika lugha ya Kiswahili. Hii itakuwa hatua kubwa hasa ikiwa masuala mbalimbali yanatafsiriwa moja kwa moja, kwa sababu watu watayapata kwa lugha ya Kiswahili mara moja na hivyo, kila mmoja atakuwa akipata ujumbe kwa haraka.

Vyombo vya habari huwa ni muhimu sana kwa watu wote. Vyombo hivyo, vina jukumu kubwa la kusambaza lugha kwa sababu watu wengi husikiliza, husoma, huangalia na kujifunza mengi. Inapendekezwa kuwa vyombo hivi vya habari visitangaze katika lugha ya makabila mengine, bali ikubaliwe lugha moja inayozungumzwa na wengi ambayo ni Kiswahili. Vyombo vya habari husambaza ujumbe kwa haraka sana. Kama vikitumiwa vibaya, vinaweza kuleta ghasia nchini. Inadaiwa kuwa mojawapo ya sababu za ghasia za baada ya uchaguzi wa mwaka 2007 ni vyombo vya habari kusambaza habari za uchochezi na uhasama. Hali hii

pia ilitokana na matumizi ya lugha za kikabila ambazo watumiaji wake aghalabu huwa na nia ya kuficha siri. Laiti lugha iliyokuwa inatumika ingekuwa Kiswahili au ingetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili, basi ghasia na fujo zingeweza kuzuiliwa na suluhu kupatikana mapema. Ni bayana kuwa ni muhimu vituo vyote vya utangazaji wa habari nchini Kenya vitangaze katika lugha inayoeleweka kwa kila mmoja ambayo ni Kiswahili au yatakayotangazwa kwa lugha nyingine yatafsiriwe ili kila mmoja aelewe kinachosemwa. Mambo yanayofichwa kwa sababu ya kutumia lugha tofauti aghalabu huleta uhasama.

Zaidi ya vyombo vya habari, kuna lugha inayotumiwa ofisini. Inapendekezwa kwamba, lugha ya ofisini iwe ni ya kila mmoja. Watu wanapozungumza ofisini waweze kuwasiliana na kuelewana. Kuna watu wengi ambao hupendelea kuongea lugha mama ofisini na hivyo hakuna kuelewana kwa watu wote. Vilevile, lugha inayotumiwa katika uwanja wa sheria, yaani Kiingereza, ni ngumu. Hii ni kwa sababu sheria hizi zilirithiwa kutoka kwa mkoloni na sera zao za uongozi. Ikabidi yale yote wanayoyafanya kule Uingereza yadhihirike katika utawala wa nchi ya Kenya. Mambo mengine yasiyoeleweka kwa mtu wa kawaida ikabidi yaingizwe vilevile. Hali hii imeleta kutoeleweka kwa sheria hizi kutokana na ugumu wa lugha ya Kiingereza ambapo mtu wa kawaida hawezi kamwe kuelewa.

Zaidi ya hayo, kutokana na ugumu wa lugha, mtu hata kama si mhalifu anaweza kupatikana na hatia kwa kujibu kitu ambacho hakielewi vizuri. Si ajabu kukuta mtu amefungwa bila hatia kwa sababu ya kutokuelewa lugha ya sheria. Lugha ya sheria inapaswa ieleweke waziwazi ili kuwe na haki kwa wanaohukumiwa. Suluhu iliyopo ni kutumia lugha ya Kiswahili.

Lugha ya Kiswahili inayoeleweka vyema inafaa itumiwe kortini na sehemu zote ambazo sheria ya nchi inatumika. Hali hii itahitaji tafsiri ya sheria zote za nchi katika lugha ya Kiswahili na katika muktadha na utamaduni wa Kiafrika, hasa Kenya. Yale ya sheria kuzingatia sera ya ukoloni yanafaa yatupiliwe mbali ili utamaduni wa Kenya udhihirike katika sheria zitakazotafsiriwa. Hili lingewezekana ikiwa Kiswahili kitatumika kwa sababu ni lugha inayofahamika kwa wengi, kwani ni lugha ya taifa nchini tangu uhuru upatikane (Chimerah, 1988). Aidha, Kiswahili katika sera za lugha kwenye mfumo wa elimu Kenya, kimekuwa kikifunzwa kama lugha tangu miaka hiyo ya sitini. Mwaka 1985, mfumo wa elimu wa 8-4-4 ulipozinduliwa nchini Kenya, baada ya Ripoti ya Tume ya Mackay ya Elimu (1982) iliyoidhinishwa na Rais Mstaafu Daniel Toritich Arap Moi, Kiswahili kilifanywa kuwa somo la lazima kutoka shule za msingi hadi sekondari. Hivi karibuni, Katiba mpya ya Kenya (2010) ilipitisha Kiswahili kuwa lugha rasmi ya pili nchini, pamoja Kiingereza; ya tatu rasmi ikiwa ni lugha ya Ishara, (Ghai, 2002). Hoja hizi hutoa sababu mwafaka kwamba Kiswahili ndiyo lugha pekee nchini Kenya kwa mawasiliano ya wengi.

Kwa upande mwingine ni muhimu kuwaelimisha watu kuhusu sheria za uchaguzi wa kisiasa. Wananchi wanapojua la kufanya hasa wakati wa uchaguzi hawataweza kuhadaiwa. Wananchi wanaweza kujua sheria hizi kupitia maelezo angavu yanayoweza kufanywa kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Sheria zilizoandikwa kwa Kiingereza zitafsiriwe katika lugha ya Kiswahili. Elimu hii ikifanywa kwa kutumia lugha ya Kiswahili itaweza kumfikia kila mmoja na pia kuleta ile hali ya umoja kati ya wananchi.

Viongozi wanaogombea nafasi mbalimbali serikalini pia wanapaswa kutoa hotuba zao kwa lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu sera zao za uongozi zinafaa zifahamike vyema kwa lugha ya wenyeji, yaani Kiswahili ndiyo itafanikisha masuala haya. Zaidi ya hayo, viongozi hawa wakitumia lugha ya Kiswahili wataweza kuhimiza umoja wa wananchi na nia moja katika majukumu yanayotakiwa kutekelezwa.

Kwa upande wa biashara, lugha ya Kiswahili inafaa isisitizwe zaidi. Hali hii inaweza kufanikishwa kwa kutafsiri mikataba ya biashara katika lugha ya Kiswahili. Shughuli za ununuzi na uuzaji wa bidhaa pia ziendeshwe kwa kutumia lugha ya wenyeji. Zaidi ya hayo, mabango ya matangazo ya biashara pia yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili ili kila mmoja ajifunze kutumia lugha ya Kiswahili na watu wote kuwa na kauli moja. Hata yale matangazo ya biashara ya redio na runinga yatafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili ili yaweze kueleweka vema kwa jamii.

Nao uwanja wa udaktari na matibabu pia unafaa uwe katika mstari wa mbele katika matumizi ya Kiswahili. Kwa mfano, madaktari, hasa wale wanaosomea nchini Kenya wawasiliane na wagonjwa wenyeji kwa lugha ya Kiswahili. Wale madaktari wanaosomea ng’ambo wanapaswa watafsiriwe masuala mbalimbali kuhusu maeneo yao tofauti ya udaktari. Maelezo ya matumizi ya dawa mara nyingi huwa yanatolewa kwa lugha zaidi ya moja ili kuweza kuwafikia watu wa lugha mbalimbali. Mara nyingi maelezo ya dawa hutolewa kwa lugha ya Kiingereza, na kutafsiriwa kwa lugha ya Kijerumani, Kifaransa, Kichina na nyingine nyingi kwa kutegemea dawa hizo zilitengenezwa wapi. Inafaa pia Kiswahili kihusishwe katika tafsiri hizo ili kwamba, kuwe na kijisehemu cha maelezo ya matumizi ya dawa kwa lugha ya Kiswahili. Jambo hili limekuwa likifanywa kwa dawa chache, lakini inapendekezwa kwamba tafsiri za maelezo kuhusu matumizi ya dawa kwa lugha ya Kiswahili zifanyike kwa dawa zote ambazo zinatumiwa nchini Kenya.

## 6.0 Hitimisho

Makala yamejadili umuhimu wa tafsiri wa kazi mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili kama njia ya kuleta umoja, uhusiano mwema na maendeleo nchini

Kenya. Yanashuhudia jinsi Kiswahili kinavyoweza kutumika kama lugha unganishi inayoweza kuleta umoja nchini. Ni lugha iliyosambaa na kutumiwa na Wakenya wengi kama lugha ya taifa takriban zaidi ya miaka 40 baada ya uhuru kama tulivyodhihirisha. Kwenye miaka ya 1980, baada ya kutambua umuhimu wa lugha hii, serikali ilitoa sera ya kukifanya Kiswahili kuwa somo la lazima kufunzwa tangu shule za msingi hadi sekondari. Jambo hili lilikiwezesha Kiswahili kupenyeza katika vitongoji vingi nchini kama inayotangamanisha watu wa makabila tofauti kitaifa na katika shughuli ya kisiasa na kibiashara. Pia matumizi rasmi ya Kiswahili yatawezesha kwa kiasi kikubwa, wasomi, wanaomudu na wasiomudu lugha ya Kiingereza, kupata taarifa zilizo sawa nchini. Endapo hatua zote zilizoelezwa katika makala haya zitazingatiwa, basi zitaweza kuchangia pakubwa hali ya umoja nchini Kenya. Lugha moja ina nguvu ya kuleta umoja na amani hasa kwenye nchi iliyo na uanuwai wa makabila na wingilugha. Utangamano, amani na umoja vitachangia ufanisi wa kimaendeleo kwa kuwa na lugha inayojumuisha watu kimawasiliano, ili kuendeleza ile nia moja ya kutekeleza masuala ya maendeleo ya nchi.

## Marejeo

Bamgbose, A. (1991). *Language and the Question in Sub-Saharan Africa.* Edinburgh: Edinburgh University Press.

Chimerah, R. (1998). *Kiswahili: Past, Present and Future Horizons*. Nairobi: Nairobi University Press.

Dion, F. (2006). Spirituality.org. za. Retrieved on 29/10/2011.

Githiora, C. (2008). *Kenya: Language and the Search for Coherent National Identity. In A. Simpson, Language and National Identity in Africa* (pp. 235-251). New York: Oxford University Press.

Ghai Y. P (2002). Taarifa ya Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya. Nairobi: Republic of Kenya. uk. vii.

Murungi, G. W. (2013). "Ufanisi Katika Pendekezo la Katiba ya Kenya". Tasnifu ya shahada ya Uzamili. Kenyatta University.(Haijachapishwa).

Roscoe, A. (1977). *Uhuru's Fire. African Literature East to South*. London: Cambridge University press.

Thiong'o N. (1993). *Decolonizing the Mind: The Politics of language in African literature*. London: James Curry and Heinemann.

Topan, F. (2008). *Tanzania*: *Development of Swahili as National and Official Language*. *In A. Simpson, Language and National Identity in Africa*. New York: Oxford University Press. pp. 256-264.

TUKI (1996). *English-Swahili Dictionary*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Tutu, D. (1999). *No Future Without Forgiveness*. New York: Doubleday, pp 294 (Book Review)

U.S. Department of State. Ubuntu Diplomacy. Retrieved on 29/10/2011.

UbuntuDeal Group Buying website opens | 2010. Retrieved on 29/10/2011.

Were, G. (2002). *Mchango wa A.S. Nabhany katika Utafiti na Utandaridhi wa Istilahi za Kiswahili*, *Utafiti wa Kiswahili Simala*, I (ed). Eldorat: Moi University Press.

Wanafunzi wa somo la tafsiri (AKS 203: Theories and Practice of Translation) Mwaka wa Pili 2011; Masomo ya Likizo.